

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Simu: +255 (738) 166 703;
Nukushi: +255 (022) 2460117
Barua pepe: secretary@psc.go.tz
Tovuti: www.psc.go.tz



6 Mtaa wa Albert Luthuli,
Kitalu Na.10,
S.L.P. 9143,
11406 DAR ES SALAAM

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma, Jaji (Mstaafu) Dkt. Steven J. Bwana, leo amehitimisha Mkutano wa Tume namba **3** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 uliofanyika Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Jaji (Mstaafu) Dkt. Bwana amesema, katika Mkutano huu Tume imetoa uamuzi wa Rufaa **151** na Malalamiko **11** yaliyowasilishwa na watumishi mbalimbali wa umma ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka zao za Ajira na Mamlaka za Nidhamu.

Kati ya rufaa **151** zilizotolewa uamuzi na Tume rufaa **82** zimekataliwa; rufaa **43** zimekataliwa kwa kuwa ziliwasilishwa nje ya muda uliowekwa kwa mujibu wa Sheria. Rufaa **12** zimekubaliwa; rufaa **11** zimekubaliwa kwa masharti kwamba zikashughulikiwe upya na Mamlaka zao za Nidhamu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Rufaa **3** hazikutolewa uamuzi kwa sababu ni kesi zilizopo Mahakamani.

Kwa upande wa malalamiko, Tume ilipokea na kutoa uamuzi wa malalamiko **11** ambapo malalamiko **6** yamekataliwa, malalamiko **4** yamekubaliwa na lalamiko **1** limekataliwa kwa sababu liliwasilishwa nje ya muda.

Imeandaliwa na:-

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Tume ya Utumishi wa Umma
DAR ES SALAAM
23 Aprili, 2021